BAJUNI

# MUONGODHO WA MWALIMU

# KIVANGO 3


Yumna Hamid Titi

Fuad Aroi

Yumbe Athman



TWAWEZA COMMUNICATIONS

Working Towards a Better World

Shungwaya Welfare Association

Umoja ni Nguvu

SWAHILI RESOURCE CENTRE

Old Town, Sir Mbarak Hinawy Road

Mombasa

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications Ltd.
Jumba la Twaweza, Barabara ya Muthithi
Mpesi Lane
S.L.P. 66872 - 00800 Nairobi, Kenya
Simu: +(254) 020 269 4409; 0727 427740
Barua pepe: info@twawezacommunications.org
Wavuti: www.twawezacommunications.org

©Haki a kunakili nḏa Twaweza Communications
Chapisho la Kwanḏa 2024

**ISBN: 978-9966-128-21-8**

Kiṯabu cha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a nradi wa kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Nradi huu huṯekeledhwa na kichuo cha Twaweza Communications, Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre. Undofadhiliwa na nfuko wa British Council Protection Fund kwa ushirikiano na UK's Department for Culture, Media and Sport.

BRITISH COUNCIL
In partnership with
Department for Culture, Media & Sport
Cultural Protection Fund

Approved by KICD

# Aliomo


1: Kuivisha Iye Na Vangine . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

2: Jamii . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

3: Vaṉama Va Mwichuni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .11

4: Usalama Barabarani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 17

5: Misimu Mbalimbali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 23


Approved by KICD

# SHUKURANI

Dhiṯabu dha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a juhudi a kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Chwaṯoa shukurani kwa mfuko wa British Council Protection Fund kwa nsaada ulochuwedhesha kuanḏika na kuchapisha dhiṯabu hidhi. Bila nsaada wavo ingalikuva ṯabu sana kuvapa vana va Kibajuni nafasi a kuifundrisha kusoma na kuanḏika Kibajuni. Chwavashukuru Dkt. Rukiya Harith na Nafisa Awadh kwa ushirikiano wavo na vaanḏishi kachika haṯua dhoṯe dha kuanḏika nfulululidho wa *Chusomeni Kibajuni*. Vaandishi va dhiṯabu hidhi – Yumna, Aroi na Yumbe – valiiṯolea kushiriki na kumalidha kuanḏika. Chwavashukuru sana kwa nchango huu muhimu. Pia chwanshukuru Athman Tora (Lalavani) na vale voṯe chufanyao navo kadhi hii adwimu a kuhifadhi na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni.

Kimani Njogu, Twaweza Communications
Omar Lali, Shungwaya Welfare Association
Athman Lali Omar, Swahili Resource Centre

Juni, 2024

Approved by KICD

# 1 KUIVISHA IYE NA VANGINE

## ISOMO LA KWANḎA

### MAḎA KURU: KUSIKIDHA

**MAḎA NDRODI: KUIELEDHA NA VANGINE**

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

a) Kudhichambua mbinu pesi dha kuieledha na kudhichumia mida a kuivisha iye na vangine.

b) Kujibu maswali akuiivisha iye na vangine kwa ufasaha.

c) Kujenga upenḏo wa kuṯaka kuiivisha na vangine.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 1

**Dhifaa dha kufundrishia:** kifaa cha kidigichali, kadi dha picha/ michoro

**Suali ḏaḏisi:** kwa nini ni muhimu kuiivisha iye na vangine?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Kushikana na hirimu ili kusikidha kaseṯi dha kuhusu namuna a kuiivisha iye na vangine.
- Kudhichambua mida na hali dha kuiivisha iye na vangine.
- Kuieledha na vangine kwa ufasaha.
- Kusikidha mazungumudho radioni uhusianao na kuieledha kwa jumula.
- Kuṯukua picha ilingamanao na mada ili kueledhea kuhusu kuiivisha na vangine.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA PILI

### MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: MADHUNGUMUDHO

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

a) Kuṯaba madhungumudho baina a vachu vawili.

b) Kufurahia maigidho a kuivishana na vangine.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 2

**Dhifaa dha kufundrishia:**Kifaa cha kidigichali, Chachi.

**Suali ḏaḏisi:** Kudhungumudha baina a vachu ṯofauṯi huecha faida gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avashirikishe vanafunḏi kaṯika makundri vajadiliane shuhuli vafanyadho vakiva ṉumbani.
- Mwalimu aṯaue vanafunḏi vavili vasome madhungumudho alioko kiṯabuni.
- Vanafunḏi kachika makundi vaṯabe madhungumudho.
- Mwalimu avavulidhe maswali kuṯokana na madhungumudho.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA CHACHU

### MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: KUSOMA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

a) Kuchambua kiini cha ujumbe kweṉe kifungu.

b) Kusoma dhifungu dhingine dhilingamanao na ujumbe wa mada.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 3

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi, kifaa cha kidigichali, kadi dha michoro/picha.

**Suali ḏaḏisi:** Ni ipi faiḏa a kusoma pweke?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Kuchambua michoro ilioko kiṯabuni.
- Kusoma kifungu cha maneno pamoya na kuunganisha dhifungu dhingine ili kupacha kiini cha ṯaarifa.
- Kusoma kwa pamoya ili kupacha kiini cha ṯaarifa.
- Kusoma pweke kisomo cha wasṯani na kujibu masuali kwa ushirikiano.
- Kuṯafudha dhifungu dha maneno kuṯoka kwa kifaa cha kidigichali.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA INE

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUUNDRA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

a) Kupanga maneno ili kuundra senchensi ilolingana na kuieledhea.

b) Kuanḏika senchensi ihusianao na ujumbe wa mada.

c) Kupumbaa kachika kuanḏika senchensi na ufasaha wa mawasiliano.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 4

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi, kifaa cha kidigichali, kadi dha maneno

**Suali ḏaḏisi:** Maneno hupangwae mpaka akaundrwa senchensi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Kushirikiana kachika kuachambua maneno ahusianao na kuiledha iye na vangine kuṯoka kwa chachi.
- Kuchumia maneno alioko kweṉe mada kwa kuanḏika senchensi kuhusu kuieledhea iye na vangine.
- Kuundra senchensi kwa kuchumia maneno alioko kweṉe kadi.
- Kuṯedha nṯedho wa kuṯoa maneno ili kuundra senchensi ihusianao na kuieledhea.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

1. Kiṯwa changu hunifuka mocho.
2. Maṯo angu hunifungia kidha.
3. Niṯafanya bidii nisirevee ṉima.
4. Sukuli iko mbali na n'yini.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

## MAḎA NDRODI: KUKAMILISHA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

a. Kuṯaua ineno sahihi kukamilisha senchensi.
b. Kuanḏika senchensi dhihusianadho na mada.
c. Kufurahia kuundra na kusoma senchensi kwa usahihi.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 4

**Dhifaa dha kufundrishia:**Kapu a maneno.

**Suali ḏaḏisi:** Maneno hupangwae mpaka akaundra senchensi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kuchambua maneno sahihi alioko kweṉe kapu a maneno.
- Vanafunḏi vasome maneno kweṉe kapu a maneno.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kuyadha senchensi.
- Vanafunḏi vasome senchensi kwa ufasaha.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopenḏekedhwa**

1. Nyalii, Bahero au....................
2. Kivango
3. Anishishie
4. Nsuaki
5. Bakhae
6. hirimu

# 2 JAMII

## ISOMO LA KWAN**D̠**A

**MAD̠A KURU: KUSIKIDHA**

**MAD̠A NDRODI: HADISI/NGANU**

**Mat̠okeo maalumu at̠arajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafund̠i awedhe;

a) Kuchambua maneno en̠e uhusiano na kadhi dha jamii.

b) Kujibu maswali kuvahusu vahusika kachika hadisi.

c) Kuchumia maneno a ubunifu kachika kueledhea hadisi a kadhi dha jamii.

d) Kujenga upendo kachika ut̠oaji wa nganu.

**Maregeleo:** Kit̠abu cha mwanafund̠i ubasho wa 5

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi, dhifaa dha kidigichali, kadi dha picha/michoro.

**Suali d̠ad̠isi:** Huvae kadhi dhikava muhimu?

**Ut̠arat̠ibu wa kufundrishia:**

- Kukusanyana kwa kusikidha nganu ihusuo kadhi kut̠oka kwa mwalimu.
- Kuchambua maneno ahusianao na kadhi dha jamii.
- Kusikidha nganu kwa dhamu dhihusidho shuhuli kachika jamii.
- Kujibu masuali kut̠oka kwa nganu.
- Kuchumia dhifaa dha kidigichali kut̠afudhia nganu.
- Mwalimu adhingat̠ie vanafund̠i ven̠e mahit̠aji maalumu.

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: KADHI MBALIMBALI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia **m**wisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kuṯaba kadhi mbalimbali.
b) Kueledha kadhi mbalimbali kachika jamii echu.
c) Kufurahia kufanya kadhi.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 6

**Dhifaa dha Kufundrishia:** kifaa cha kidigichali,chachi**.**

**Suali ḏaḏisi:** Ni kadhi gani dhifwanyadho kachika maeneo echu**?**

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vaongodhe vanafunḏi kuchaya kadhi ambadho vadhipenḏadho.
- Vaavanye vanafunḏi kachika makundri mbalimbali.
- Liongodhe ikundri imoya imoya kuṯaba shuhuli dha kadhi hidho.
- Vapongedhe vanafunḏi kwa kushiriki kachika maigidho hao.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: KUSOMA KWA SAUṮI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kusoma nganu kwa ufasaha.
b) Kuaṯamuka maneno ahusianao na mada kwa ufasaha .
c) Kujenga upenḏo wa kusoma kwa ufasaha.


Approved by KICD

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 7

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi, dhifaa dha kidigichali, kadi dha picha/michoro

**Suali ḏaḏisi:** Kusoma kwa sauṯi kunao faida gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Kushirikiana na hirimu kachika kusoma nganu pesipesi dhilingamanao na mada.
- Kushirikiana pamoya kachika kuṯamuka maneno sawasawa ahusianao na kadhi sawa na shuhuli dha jamii.
- Kuiorodhesha kusoma kwa sauṯi kwa kushirikiana na hirimu.
- Kuṯaua dhiṯabu dha nganu dhifaadho na kudhisoma kwa sauṯi.
- Kuṯafudha dhifaa dha kidigichali kwa lengo la kupacha nganu dha kusomwa.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopenḏekedhwa**

1. Hadhigi ni mweṉe kuṯibu vachu, mfano wa dakiṯari.
2. Mayembe, dhisalima na dhiṯoka.
3. Valisoma kwa bidii.
4. Kupacha maisha madhuri.
5. Mabochi makuru.

## ISOMO LA INE

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI : KUUNDRA HARUFU

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuchaya harufi dha maneno kachika senchensi.

b) Kuanḏika kwa udhuri na kuanḏama harufu kwa dhipambodhe.

c) Kujenga upend̠o kwa kuand̠ika maneno mafupi mafupi.

**Maregeleo:** Kit̠abu cha mwanafund̠i ubasho wa 8

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi, dhifaa dha kidigichali.

**Suali d̠ad̠isi:** Ut̠aundrae ineno kuchumia harufu?

**Ut̠arat̠ibu wa kufundrishia:**

- Kut̠aba na kusinanga harufu.
- Kuand̠ika kwa udhuri wa mavumbo na kuat̠ana kwa hat̠ua dhake.
- Kusoma nganu fupifupi na pesi pamoya na kuchambua kiini cha ujumbe.
- Kuand̠ika maneno kupichia maneno vapawao na mwalimu (hadhigi, rubani, nkulima, nt̠onyi)
- Kuand̠ika nganu kwa kuchumia maneno mafupi ahusianao na shuhuli dha jamii.
- Kudhundrua maarifa a kuundra nganu fupi fupi dha kupendedha.
- Mwalimu adhingat̠ie vanafund̠i ven̠e mahit̠aji maalumu.

## ISOMO LA T̠ANU

## MAD̠A KURU: KUAND̠IKA

## MAD̠A NDRODI: HAT̠I

**Mat̠okeo maalumu at̠arajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafund̠i awedhe:

a) Kuand̠ika senchensi dhilidhoko kit̠abuni kwa hat̠i nadhifu.

b) Kuand̠ika senchensi fupifupi en̠e nsingi wa mada.

c) Kufurahia kuand̠ika na kuchunga senchensi kwa udhuri kulingana na picha.

**Maregeleo:** Kit̠abu cha mwanafund̠i ubasho wa 9


Approved by KICD

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chachi, michoro

**Suali d̲ad̲isi:** Nchungo ndhuri huand̲ikwae?

**Ut̲arat̲ibu wa kufundrishia:**

- Kushirikiana kachika kuachambua maneno a kuiledhea kut̲oka kwa chachi.
- Kuvaongodha vanafund̲i vaand̲ike senchensi dhilidhoko kit̲abuni kwa hat̲i nadhifu.
- Vashirikishe vanafund̲i vajadili picha kit̲abuni.
- Vaongodhe vanafund̲i vaand̲ike nchungo kuhusu picha valopawa.
- Soma nchungo wa vanafund̲i kadhaa ili kuwedha kurekebisha.
- Mwalimu adhingat̲ie vanafund̲i ven̲e mahit̲aji maalumu.

# 3 VAN̠AMA VA MWICHUNI

## ISOMO LA KWAND̠A

### MAD̠A KURU: KUSIKIDHA

### MAD̠A NDRODI: DHILIO DHA VAN̠AMA VA MWICHUNI

**Mat̠okeo maalumu at̠arajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafund̠i awedhe:

a) Kuchaya maina a van̠ama va mwichuni.

b) Kudhichambua saut̠i dha van̠ama mbalimbali va mwichuni.

**Maregeleo:** Kit̠abu cha mwanafund̠i ubasho wa 10

**Dhifaa dha kufundrishia:** Picha dha van̠ama, kifaa cha kidigichali.

**Suali d̠ad̠isi:** Van̠ama va mwichuni huchusaidia nini?

**Ut̠arat̠ibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avavulidhe masuali vanafund̠i kuhusu van̠ama va mwichuni k.m: nn̠ama hat̠ari mwichuni ni upi?
- Vanafund̠i vadhungumudhe kuhusu van̠ama.
- Mwalimu avasikidhishe saut̠i mbalimbali dha van̠ama akichumia kifaa cha kidigichali, vanafund̠i vadhichambue saut̠i hidho.
- Vaongodhe kuangalia picha ubasho wa 10 vachaye maina a van̠ama.
- Vashirikishe vanafund̠i kut̠aba saut̠i dha van̠ama na vangine vadhichambue.
- Vanafund̠i vachore nn̠ama wa mwichuni vampend̠ae.
- Mwalimu adhingat̠ie vanafund̠i ven̠e mahit̠aji maalumu.


Approved by KICD

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: UMUHIMU WA VAṈAMA VA MWICHUNI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuṯoa ujumbe kwa kuchumia picha dhilidhoko kiṯabuni.

b) Kuchaya maina a vaṉama na umuhimu wavo.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 11

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi maneno, kifaa cha kidigichali.

**Suali ḏaḏisi:** Vaṉama va mwichuni vana umuhimu gani kwechu?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vakumbuse vanafunḏi kuhusu vaṉama va mwichuni valivosoma kachika isomo lilopicha.
- Vaongodhe vanafunḏi kuangalia picha dhiṯabuni kueledhea vakivonacho.
- Vape nafasi vanafunḏi vajalidiliane kuhusu umuhimu wa vaṉama va mwichuni kachika dhikundri.
- Orodhesha umuhimu wa vaṉama va mwichuni ubavoni vanafunḏi vasome kwa sauṯi.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: KULINDRA VAṈAMA VA MWICHUNI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuchaya sampuli mbalimbali dha kuvalindra vaṉama va mwichuni.

b) Kueledha umuhimu wa vaṉama va mwichuni.

c) Kufurahia kuvalindra vaṉama va mwichuni.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha vanafunḏi ubasho wa 11

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chachi, kifaa cha kidigichali

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vashirikishe vanafunḏi kukumbuka umuhimu wa vaṉama va mwichuni.
- Vaveke vanafunḏi kachika dhikundri vachaye namuna a kuvahifadhi vaṉama va mwichuni.
- Vanafunḏi vasome maeledho kachika chachi.
- Vanafunḏi vakaṯafudhe nḏia dhaiḏi dha kuvalindra vaṉama va mwichuni.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA IṈE

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: HIFADHI DHA VAṈAMA VA MWICHUNI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuchaya namuna mbalimbali dha kuhifadhi vaṉama va mwichuni.

b) Kusoma madhungumudho na kujibu masuali.

c) Kufurahia kusoma madhungumudho.

**Marejeleo:**Kiṯabu cha vanafunḏi ubasho wa 11 na 12.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Picha dha vavindaji na vaṉama, kifaa cha kidigichali.

**Suali ḏaḏisi:** Kwa nini vanafunḏi hupekwa maṯembedhi kweṉe hifadhi a vaṉama va mwichuni?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kueledhea kuhusu picha.
- Vanafunḏi vachaye vaṉama vavindrwavo.
- Vanafunḏi vasome madhungumudho kiṯabuni.
- Vanafunḏi vaeledheane kuhusu madhungumudho.
- Vanafunḏi vajibu masuali.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

**MAḎA NDRODI: KUUNDRA SENCHENSI**

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kupanga maneno kuundra senchensi sawa.

b) Kusoma senchensi kwa udhuri.

c) Kufurahia kuundra na kusoma senchensi.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 14.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi maneno, Chachi

**Suali ḏaḏisi:** Senchensi huundrwaye?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vaongodhe vanafunḏi kusoma maneno kwa usawa.
- Vanafunḏi vasome maneno kachika kadi dha maneno.
- Vaongodhe kuchumia kadi maneno kupanga senchensi.
- Vaongodhe kusoma senchensi kwa sauṯi.
- Vanafunḏi vaundre senchensi zaiḏi dhiṯabuni.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

1. Makadhi a vaṉama
2. simba, nachi, ṯuvi, pisi
3. simba
4. Vasivuwawe, huecha senṯi dha kigeni.
5. majangili

## ISOMO LA SIṮA

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

## MAḎA NDRODI: KUCHUNGA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuchunga senchensi kuhusu ulindraji wa vaṉama pori.

b) Kusoma senchensi kwa udhuri

c) Kufurahia kuchunga na kusoma senchensi.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 14

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi maneno

**Suali ḏaḏisi:** Mfalume wa vaṉama va mwichuni ni nyanyi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vaongodhe vanafunḏi kusoma maneno kweṉe kadi.
- Vaongodhe vanafunḏi vapange maneno kuchengedha senchensi.
- Mwalimu avasaiḏie vanafunḏi kuundra senchensi.
- Vanafunḏi vasome senchensi kwa sauṯi.
- Vanafunḏi vaanḏike senchensi dhiṯabuni.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

# 4 USALAMA BARABARANI

**ISOMO LA KWANḎA**

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: HADISI**

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kusimulia hadisi.

b) Kusikidha hadisi.

c) Kufurahia kusimulia na kusikidha hadisi.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 16.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhiṯabu dha hadisi, Kifaa cha kidigichali.

**Suali ḏaḏisi:** Kwa nini chwaṯakiwa chuve vaangalifu barabarani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kueledha umuhimu wa kuva makini barabarani.
- Vanafunḏi vajaḏili nchoro ulioko kiṯabuni ubasho wa 16.
- Mwalimu asimulie hadisi fupi kuhusu usalama wa barabarani.
- Aagidhe vanafunḏi vasimuliane hadisi fupifupi kachika makundri.
- Mwalimu avase kifaa cha kidigichali na avaagidhe vanafunḏi vaṉamae ili vasikidhe hadisi kwa uchulivu.
- Mwalimu avavudhe masuali kuṯokana na hadisi valosikidha.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.



Approved by KICD

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: USHAIRI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kufikia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kusoma shairi.

b) Kukariri shairi kwa mahadhi.

c) Kufurahia kusoma na kukariri shairi.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 17.

**Dhifaa dha Kufundrishia:** Chachi, Kifaa cha kidigichali

**Suali ḏaḏisi:** Ni alama gani vachu hufaa kuvuka kachika barabara?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi masuali kuhusu barabara.
- Mwalimu asome shairi na alikariri kwa mahadhi.
- Vaagidhe vanafunḏi vafungue ubasho wa 17 ili vasome shairi kwa sauṯi.
- Vanafunḏi vanṯabe mwalimu akikariri shairi.
- Angika chachi ubavoni, vanafunḏi vachambue alama a pundra milia.
- Vaeledhe umuhimu wa alama hiyo.
- Hiṯimisha isomo kwa kueledhea ujumbe umuhimu kweṉe shairi hilo.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: UFAHAMU (SHARIA DHA BARABARANI)

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:-

a) Kusoma ufahamu kwa udhuri.

b) Kujibu masuali a ufahamu.

c) Kufurahia kusoma ufahamu.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 18.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kifaa cha kidigichali, Chachi.

**Suali ḏaḏisi:** Ni sharia gani dha barabarani udhiyivadho?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kuregelea isomo lililopicha kwa kuvavulidha vanafunḏi masuali kuhusu usalama barabarani.
- Vaagidhe vanafunḏi vafungue dhiṯabu ubasho wa 18 ili vajaḏili picha.
- Mwalimu asome kifungu cha kwanḏa kwa sauṯi.
- Vaagidhe vanafunḏi vasome ufahamu kwa sauṯi.
- Angika chachi ubavoni na aeledhe umuhimu wa ṯaa dha barabara.
- Ahiṯimishe isomo kwa kuvaagidha vanafunḏi vajibu masuali.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

1. Makini, ṯahadhari, mwangalifu.
2. Kulia na kusoṯo.


Approved by KICD

3. Daraja la kuvukia, kuvuka kweṉe alama dha pundra milia, kuangalia michoro a ṯahadhari.
4. Leseni.
5. Maovu.

## ISOMO LA IṈE

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: KUSOMA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kusoma senchensi kwa udhuri.

b) Kufurahia kusoma senchensi.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 20.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chachi.

**Suali ḏaḏisi:** Ni sehemu gani salama dha kuvuka barabara?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kuvavulidha vanafunḏi masuali kuhusu barabara.
- Mwalimu aagidhe vanafunḏi vafungue ubasho wa 20.
- Mwalimu asome senchensi kwa sauṯi na vanafunḏi vamuanḏame akisoma.
- Kachika makundri, vanafunḏi vasome senchensi hidho kwa sauṯi.
- Hiṯimisha isomo kwa kuangika chachi ubavoni ili vanafunḏi vasome.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA ṮANU

### MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUANḎIKA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kuanḏika senchensi kwa udhuri.

b) Kufurahia kuanḏika senchensi.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 20

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi maneno

**Suali ḏaḏisi:** Ni alama dhipi dha barabarani udhiyivadho?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avashirikishe vanafunḏi vasome maneno kweṉe kadi.
- Mwalimu aundre senchensi kuchumia ineno imoya kweṉe kadi na alianḏike ubavoni.
- Avaagidhe vanafunḏi vafungue dhiṯabu ubasho wa 20 vasome hao maneno.
- Vanafunḏi vachunge senchensi vakichumia maneno hao.
- Hiṯimisha isomo kwa kurekebisha senchensi hidho pamoya na vanafunḏi.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA SIṮA

### MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUANḎIKA NCHUNGO

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kuanḏika nchungo ndhuri.

b) Kufurahia kuanḏika nchungo.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 20

**Dhifaa dha Kufundrishia:** Kifaa cha kidigichali

**Suali ḏaḏisi:** Nchungo ni nini?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kueledha maana a nchungo.
- Mwalimu avaeledhe namuna a kuanḏika nchungo weṉe nṯiririko ndhuri na wa kueleweka.
- Avase kifaa cha kidigichali avavoneshe vanafunḏi nfano wa nchungo ndhuri.
- Avaagidhe vaanḏike nchungo kuhusu usalama barabarani.
- Hiṯimisha isomo kwa kusisiṯidha vaanḏike misemo na mesali kweṉe nchungo.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu

# 5 MISIMU MBALIMBALI

## ISOMO LA KWANḎA

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: MISIMU MBALIMBALI**

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kuchambua misimu mbalimbali kachika mwaka.

b) Kuchaya shuhuli dhifanywadho kachika misimu mbalimbali.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 21

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chachi, kifaa cha kidigichali, kadi maneno

**Masuali ḏaḏisi**: Misimu ni nini? Uṯachambuaye misimu mbalimbali a mwaka?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avaavanye vanafunḏi kwa dhikundri.
- Vaongodhe vanafunḏi kudhungumudha kuhusu picha dhiṯabuni ubasho 21.
- Vanafunḏi vaeledhane alioko kweṉe picha.
- Mwalimu avachayie misimu mbalimbali akichumia kadi maneno.
- Vanafunḏi vachambue misimu mbalimbali na shughuli dhifanyikadho kachika kila nsimu.
- Vanafunḏi vaimbe nyimbo ichayadho misimu.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: NJAḎALA

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuchaya faida dha nsimu wa vua na yuva.

b) Kushiriki kachika njadala.

c) Kufurahia kushindrana kachika njadala.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho 22

**Dhifaa dha kufundrishia**: kadi maneno, kifaa cha kidigichali

**Suali ḏaḏisi**: Njadala ni nini? Njaḏala hufanywaye?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avavulidhe vanafunḏi kueledha maana a njaḏala. Vanafunḏi vaeledheane.
- Mwalimu afafanue dhaiḏi maana a njaḏala.
- Avasikidhishe njaḏala kachika kifaa cha kidigichali.
- Vaavanye vanafunḏi kachika makundri mavili vajadili njadala 'nsimu wa vua ni bora kuliko wa yuva'.
- Vanafunḏi vajadiliane na kushindrana vakifuacha masharuṯi a njaḏala.
- Mwalimu avasifu vanafunḏi valivoshiriki na avahimidhe vangine vashiriki kachika njaḏala.
- Mwalimu adhisome hoja dha vanafunḏi. Vanafunḏi vadhisome kwa sauṯi.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: UFAHAMU

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kusoma kwa sauṯi.

b) Kujibu masuali a ufahamu.

c) Kusoma kwa udhuri na kufurahia.

**Suali ḏaḏisi**: Ni shuhuli gani hufanywa kweṉe misimu mbalimbali?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 22-23.

**Dhifaa dha kufundrishia**: Kadi dha misimu, Chachi, kadi maneno

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kuvakumbusa vanafunḏi kuchaya misimu mbalimbali.
- Mwalimu avaeledha vanafunḏi namuna a kuva nsomi ndhuri.
- Vaeledhe uṯaraṯibu wa kusoma kwa udhuri.
- Vaagidhe vanafunḏi kufungua ubasho wa 22-23, Vape muda vadhungumudhe kuhusu picha.
- Vaongodhe kusoma kwa udhuri kimwakimwa. Kisha vasome kwa sauṯi vakipokedhanya.
- Vasaidie vanafunḏi kuchambua maneno mapiya, vaeledhe maana ake.
- Chumia kadi maneno kuvavonesha vanafunḏi maneno mapiya.
- Vasifu vanafunḏi na uvahimidhe kupenḏa kusoma.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.



Approved by KICD

**Majibu alopendekedhwa**

1. Ni kipindri kachika mwaka ambapo hali maalumu a hewa hupachikana.
2. Nsimu wa kiangadhi/yuva, kusi/vua, dhoruba/upepo, vua rasharasha.
3. Nsimu wa dhoruba/upepo
4. Kusi/vua
5. Baridi kali

## ISOMO LA IN̠E

## MAD̠A KURU: KUSOMA

### MAD̠A NDRODI: KUSOMA SENCHENSI

**Mat̠okeo maalumu at̠arajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafund̠i awedhe:

a) Kusoma senchensi kwa udhuri

b) Kuchaya misimu mbalimbali

**Suali d̠ad̠isi**: Ni shuhuli gani hufanyika nsimu wa vua?

**Maregeleo:** Kit̠abu cha mwanafund̠i ubasho wa 23

**Dhifaa dha kufundrishia**: Kadi dha senchensi

**Ut̠arat̠ibu wa kufundrishia:**

- Changulidha kwa kuvaelekedha vanafund̠i mambo a kudhingat̠ia wakat̠i wa kusoma.
- Vashirikishe vanafund̠i kachika kusoma senchensi.
- Kachika dhikundri vanafund̠i vasome senchensi kuchumia kadi maneno.
- Vanafund̠i vasome senchensi kwa saut̠i dhit̠abuni ubasho wa 23.
- Vahimidhe vanafund̠i kupend̠a kusoma mara kwa mara.
- Mwalimu adhingat̠ie vanafund̠i ven̠e mahit̠aji maalumu.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: NRABA

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kukamilisha nraba.

b) Kufurahia kuyadha nraba.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 24

**Dhifaa dha kufundrishia**: Nraba, kadi dha misimu

**Suali ḏaḏisi:** Ni nsimu gani upendwao na vakulima?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vashirikishe vanafunḏi kuchaya misimu valosoma kipindri cha ṉima.
- Vavoneshe vanafunḏi kadi dheṉe misimu mbalimbali.
- Vaongodhe vanafunḏi kuangalia nraba ubasho wa 24. Vape maagidho a namuna a kuchambua maneno a misimu.
- Vanafunḏi vaṯafudhe maina a misimu kachika nraba.
- Vapongedhe vanafunḏi valivowedha kupacha maina oṯe mara moya.
- Rudia misimu oṯe pamoya na vanafunḏi kweṉe nraba.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu Alopenḏekedhwa:**

| | |
|---|---|
| 1. Kusi | 2. Kiangadhi |
| 3. Chaka | 4. Dhoruba |
| 5. Maṯlai | |



Approved by KICD

## ISOMO LA SIṮA

## MAḒA KURU: KUANḒIKA

### MAḒA NDRODI: NCHUNGO

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kuanḏika nchungo ndhuri.

b) Kufurahia kuanḏika nchungo.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 24.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chachi, mifano a michungo

**Suali ḏaḏisi:** Ni nsimu gani vaṉama hudhoofika nno?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vaeledhe shuhuli dha misimu mbalimbali.
- Vasomee mifano a michungo mbalimbali.
- Vaanḏikie dhipengee mbalimbali kuhusu misimu.
- Kachika makundri vajadiliane dhipengee na vaanḏike nchungo kwa kusaidiana.
- Vape muda vanafunḏi vasome michungo avo mbee a darasa
- Rekebisha makosa a vanafunḏi.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.